TANGAZO LA SERIKALI NA. 918 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kam muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"bidhaa" maana yake ni kitu chochote chenye thamani kitakacholetwa sokoni kwa lengo la kuuzwa;

"bucha" maana yake ni jengo au duka maalumu kwa ajili ya kuuzia nyama lenye vigezo vinavyokubalika kisheria;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu, au mizigo

kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa, mkokoteni, au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"ghala" maana yake ni jengo au sehemu iliyotengwa kwa ajili ya kazi ya kuhifadhi mazao au bidhaa nyingine yoyote inayoweza kuuzwa

"gulio" maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati maalumu kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"kibanda" maana yake ni jengo au chumba cha biashara;

"leseni" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, kampuni au taasisi kinacho ruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri;

"machinjio'' maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa lengo la kuchinja mifugo;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda maalum;

"magogo" maana yake ni miti iliyokatwa yenye unene zaidi kipenyo cha sentimita ishirini na kuendelea yanayotarajiwa na yenye mwelekeo wa kutoa mbao na bidhaa nyingine;

"mali za Halmashauri" maana yake ni miliki zote za kudumu na za muda za Halmashauri pamoja na nyumba, kumbi, magari, mitambo na vibanda vya Halmashauri;

"mazao" maana yake ni mazao yote ya chakula au biashara au maua au matunda na mboga yanayolimwa ndani na nje ya Halmashauri;

"meza" au "kizimba" maana yake ni kitu au kifaa

kinachotambulika kwa namba au alama kinachotumika kuwekea bidhaa za biashara katika soko au eneo lililoidhinishwa na Halmashauri;

"mifugo" maana yake ni wanyama wote wafugwao na binadamu na itajumuisha nyuki, samaki, bata na kuku;

"mnara" maana yake ni kifaa kinachopokea na kusafirisha mawasiliano ya simu au redio isipokuwa mnara unaotumika kuongoza vyombo vya usafiri;

"mkaa" maana yake ni miti iliyochomwa na kukusanywa kwa pamoja kwa ajili ya matumizi ya kupikia pamoja na shughuli nyingine;

"mkataba" maana yake ni makubaliano yenye nguvu ya kisheria ya ununuzi au uuzaji au Utoaji wa huduma yoyote kati ya Halmashauri na wadau wa Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni eneo maalumu lililotengwa na kumilikiwa na Halmashauri kwa ajili ya biashara ya kuuza na kununua bidhaa au huduma kufuatanana taratibu zilizowekwa na Halmashauri;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa shughuri za kuuza na kununua bidhaa;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia au kushusha abiria na mizigo;

"usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kutambua na kuorodhesha vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni tozo inayotozwa au

kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa Kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara, mtoa huduma au mtu yeyote mwenye leseni ya biashara kwa huduma anazopata kutokana na kutumia miundombinu ya Umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali au leseni au huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada au ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Ushuru wa huduma

5.-(1) Halmashauri itakusanya na kutoza ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kutoka kwa kila kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara, mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara na mtoa huduma yeyote kwa kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika au kutolewa ndani ya eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya bidhaa (excise duty).

(2) Mfanyabiashara mwenye leseni ya biashara ambae ameshindwa kutunza kumbukumbu na hakuna namna ya kupata taarifa zake atalipa ushuru kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

6. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

7.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na baada ya kukamilisha malipo mlipaji atapewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa.

Ukusanyaji wa madeni

8. Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi au kikundi au taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu

kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama

(5) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

9.-(1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

10. Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

11.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu au vitabu au hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa au atadharau au atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au

(g) atatengeneza au atatayarisha au ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Adhabu

12. Mtu atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii na kutiwa hatiani atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 110 la 2008

14. Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Kibondo ya Mwaka 2008 imefutwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1) na 5(2))*

SEHEMU YA I: UKODISHAJI AU UPANGISHAJI WA MALI ZA HALMASHAURI

| Namba. | Aina ya tozo | kiasi cha tozo (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba. |
| 2. | Magari ya Halmashauri | kwa mujibu wa mkataba. |
| 3. | Kumbi za Halmashauri | 300,000/= kwa siku. |
| 4 | Viwanja vya wazi vya Halmashauri | 50,000/= kwa siku. |
| 5 | Vibanda vya biashara (kwa mwezi) | kwa mujibu wa mkataba. |
| 6 | Vifaa na Magari | kwa mujibu wa makubaliano. |
| 7 | Vizimba | kwa mjibu wa mkataba. |

SEHEMU YA II: USHURU WA SOKO, KUSHUSHA NA KUPAKIA MIZIGO

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari ndogo la mizigo | 10,000/= kwa kila gari. |
| 2 | Gari kubwa la mizigo | 20,000/= kwa kila gari. |
| 3 | Dumu la mawese lita 20 | 500/= kila dumu. |
| 4 | Dagaa | 1,000/= kwa kila gunia. |
| 5 | Samaki | 2,500/= kwa kila tenga/boksi. |
| 6 | Kuingiza sokoni Gunia, Tenga, Robota la mitumba na Kiloba<br>Tafsiri ya Tenga<br>- Tenga tikiti 15<br>- Tenga nanasi 35<br>- Tenga la fenesi 10<br>- Tenga la staferi 50<br>- Tenga la maboga 15<br>- Mzigo wa miwa 10<br>- Masanduku ya mbao ya kubebea nyanya | 500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Mama lishe au Baba lishe | 500/= |
| 8 | Eneo la matenga | 500/= |
| 9 | Ada ya eneo la machinjio ya kuku | 500/= kwa kila mtu. |
| 10 | Maegesho Sokoni | 500/= kwa siku. |
| 11 | Dalali | 1,000/= kwa kila mtu. |
| 12 | Gulio | 500/= kwa kila mtu. |
| 13 | Fundi nguo kwa cherehani | 500/= kwa kila mtu. |
| ANGALIZO: Maeneo ya kushusha na kupakia mizigo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ni kama ifuatavyo:<br><br>Soko kuu la Kibondo mjini, stendi ya Maroli, soko la mikaratusini, soko la Mabamba, soko la ujirani Mwema Mkarazi, Kibuye, Kigina, Nyaruyoba, Kifura, mnada na maeneo mengine yatakayotengwa na Halmashauri kama maeneo ya kushusha na kupakia mizigo. | | |

SEHEMU YA III: USHURU WA MATANGAZO AU SANAA AU TAMASHA

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Vibali vya matamasha ya ngoma au nyimbo au muziki | 30,000/= kwa kibali. |
| 2. | Maombi ya kibali cha kufanya sanaa au maonyesho au kumbi za picha jongefu | 10,000/= kwa siku. |
| 3. | Maombi ya kibali cha kupiga disko au dansi | 35,000/= kwa siku. |
| 4. | Matangazo kwa kutumia kipaza sauti | 350,000/= kwa siku. |
| 5. | Maombi ya kibali cha kufanya sherehe | 10,000/= kwa siku. |
| 6. | Kuendesha mikutano ya hadhara ya Injili | 10,000/= kwa siku. |
| 7. | Kuuza miziki ada ya usajili wa vikundi vya sanaa | 25,000/= kwa siku. |
| 8 | Ada za kumbi za starehe na mikutano | 25,000/= kwa siku. |
| 9 | Ada ya ukaguzi wa mihtasari ya Halmashauri | 10,000/= kwa kila Muhtasari. |

SEHEMU YA IV:

(a) Ushuru wa Maegesho Stendi ya mabasi au Probox au Malori na Maeneo mengine ya Halmashauri

| Namba. | Aina ya chanzo | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari binafsi | 500/= kwa siku. |
| 2 | Pikipiki | 500/= kwa wiki. |
| 3 | Gari ndogo | 500/= kwa siku. |

| | | |
|---|---|---|
| 4 | Teksi | 500/= kwa siku. |
| 5 | Gari ndogo ya abiria | 1,500/= kwa siku. |
| 6 | Gari kubwa ya abiria | 3,000/= kwa siku. |
| 7 | Lori lenye uzito zaidi ya tani saba (7) | 5,000/=kwa siku. |
| 8 | Malori lenye uzito chini ya tani saba (7) | 3,000/= kwa siku. |
| 9 | Ada ya kutunza gari ililokamatwa au kuzuiliwa lenye uzito chini ya tani saba | 10,000/= kwa siku. |
| 10 | Ada ya kutunza gari ililokamatwa au kuzuiliwa lenye uzito zaidi ya tani saba | 20,000/= kwa siku. |

(b) Ada ya Usajili Vyombo vya Usafiri

| NA. | Aina ya chanzo | Kiwango ch Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki/ | 5,000/= kwa mwaka. |
| 2 | Bajaji | 10,000/= kwa mwaka. |
| 3 | Gari dogo la mizigo | 50,000/= kwa mwaka. |
| 4 | Teksi | 50,000/= kwa mwaka. |
| 5 | Gari lenye uwezo wa kubeba abiria chini ya 25 | 70,000/= kwa mwaka. |
| 6 | Gari lenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 25 | 100,000/= kwa mwaka. |
| 7 | Lori lenye uzito chini ya tani 7 | 100,000/= kwa mwaka. |
| 8 | Lori lenye uzito zaidi ya tani 7 | 150,000/= kwa mwaka. |

## SEHEMU YA V:

### A. Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa Nyama

| Namba. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | 5,000/= kwa kila mmoja. |
| 2 | Kondoo au Mbuzi | 1,500/= kwa kila mmoja. |
| 3 | Nguruwe | 2,500/= kwa kila mmoja. |
| 4 | Cheti cha usafirishaji wa ngozi za wanyama zilizotengenezwa tayari kwa kuuzwa. | 3,000/= kwa cheti kimoja. |
| 5 | Ukaguzi wa mifugo | 10,000/= kila mwezi anapoenda kukagua mifugo. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Chanjo kwa Ng'ombe | 550/= kwa kila Mmoja |

B. Ada Nyinginezo za Huduma ya Mifugo

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi). |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kutunza Ng'ombe mmoja machinjioni kwa siku | 1,000/= |
| 2. | Ada ya kutunza Mbuzi au Kondoo mmoja machinjioni kwa siku | 500/= |
| 3. | Ada ya soko au mnada wa mifugo | 1,000/=kwa kila mfugo |
| 4. | Ada ya machinjio ya kuku | 500/= kwa kila mmoja |

C. Vibali vya kusafilisha mifugo

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi). |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe au mbuzi na kondoo | 10,000/= kwa kila kibali. |
| 2. | Wanyama wengine | 5,000/= kwa kila kibali. |
| 3. | Leseni za usafirishaji ngozi na ngozi za wanyama zilizotengenezwa tayari kwa kuuzwa | 150,000/= leseni moja kwa mwaka. |

SEHEMU YA VI: USHURU WA VYOO VYA UMMA

| Namba. | Aina ya chanzo | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi). |
|---|---|---|---|
| 1. | Choo cha Sokoni | Kuoga | 500/= |
| | | Haja ndogo | 300/= |
| | | Haja kubwa | 300/= |
| 2. | Choo cha Stendi | Kuoga | 500/= |
| | | Haja ndogo | 300/= |
| | | Haja kubwa | 300/= |
| 3. | Maeneo mengine | Kuoga | 500/= |
| | | Haja ndogo | 300/= |
| | | Haja kubwa | 300/= |

SEHEMU YA VII: USHURU WA VIWANDA VYA MATOFALI

| Namba. | Aina ya chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maeneo ya mjini | 100,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 918 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Maeneo ya pembezoni | 50,000/= |

SEHEMU YA VIII: USHURU WA KUHIFADHI MAZAO GHALANI NA KUSAFIRISHA MAZAO MBALIMBALI ZAIDI YA TANI MOJA

| Namba | Aina ya chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mihogo | 1,500/= kwa gunia ilisilozidi kilo 100. |
| 2. | Alizeti au karanga na mazao mengine jamii ya kunde | 2,000/= kwa gunia. |
| 3. | Miwa tani moja | 15,000/=kwa tani moja. |
| 4. | Chia | 2,000/= kwa kila debe. |
| 5. | Dumu la alizeti lita 20 | 2,000/= kwa kila dumu. |
| 6 | Mashudu | 2,000/= kwa kila gunia. |
| 7. | Mahindi au mtama na mazao ya nafaka | 2,000/= kwa gunia. |
| 8. | Kuhifadhi mazao katika ghala ndogo | 25,000/= kwa kila mwaka. |
| 9. | Kuhifadhi mazao katika ghala kubwa | 50,000/= kwa kila mwaka. |
| 10. | Chumvi | 2,000/= kwa gunia. |
| 11. | Matunda | 1,000/= kwa gunia. |
| 12. | Mkaa | 1,000/= kwa gunia. |
| 13. | Mbao | 500/= kwa kila ubao. |
| 14. | Mirunda | 1,000/= kwa kila gogo. |
| 15. | Ndoo ya Asali masega au chujiwa | 3,000/= kwa kilo 10 hadi 20. |
| 16. | Nta na mazao mengine ye nyuki | 500/= kwa kilo. |
| 17. | Ushuru wa kukamua alizeti | 1,000/= kwa siku. |
| 18. | Ushuru wa kukoboa mpunga na kusaga mahindi | 1,000/= kwa siku. |

SEHEMU YA IX: USHURU WA KUSAFIRISHA MAZAO YA MISITU YA ASILI NA YA KUPANDWA

A. Misitu

| Namba | Aina ya chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Kukata au kukusanya au kusafirisha nishati ya kumi. | 2,500/=kwa mita moja ya ujazo |
| 2 | Kukata na kusafirisha magogo ya futi 7 hadi 10 ya miti ya kupandwa | 2,000/=kwa kila gogo |
| 3 | Kukata au kusafirisha fito au nguzo za miti ya kupandwa fito au nguzo | 500/= kwa kila fito au nguzo |
| 4 | Kupasua na kusafirisha mbao zinazotokana na miti ya kupasua | 500/=kwa kila ubao |
| 5 | Kukata na kusafirisha magogo ya miti ya asili italipwa | 5% ya tozo za TFS. |
| 6 | Kukata na kusafirisha fito au nguzo za miti ya asili italipwa | 5% ya tozo za TFS. |
| 7 | Kupasua na kusafirisha mbao zinazotokana na miti ya asili italipwa | 5% ya tozo za TFS. |

B. Utunzaji wa Mazingira

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Mwekezaji wa mradi | Atalipia 6% ya gharama aliyolipia tathmini ya athari kwa mazingira. |

SEHEMU YA X: ADA YA MAOMBI YA KUJENGA VITUO VYA KUOSHEA MAGARI

| Namba | Aina ya chanzo | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maeneo ya katikati ya mji | 20,000/= kwa mwaka. |
| 2. | Nje ya maeneo ya katikati ya mji | 10,000/= kwa mwaka. |
| 3. | Maeneo mengine wa Vijijini | 5,000/=kwa mwaka. |

SEHEMU YA XI: ADA YA UKAGUZI WA AFYA

| Namba | Eneo la Ukaguzi | Kiwango cha Ada (Shilingi.) Kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= |
| 2. | Mighahawa | 2,000/= |
| 3. | Bucha. | 2,000/= |
| 4. | Vibanda au maeneo ya kuchomea nyama au kukaanga. Chipsi au | 2,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | nyama au mayai. | |
| 5. | Hoteli. | 10,000/= |
| 6. | Kumbi za muziki (disko au dansi) au Baa. | 5,000/= |
| 7. | Vibanda vya biashara na maeneo ya biashara nyinginezo. | 3,000/= |
| 8. | Ghala ya bidhaa za vyakula vinywaji . | 5,000/= |
| 9. | Nyumba za makazi. | 1,000/= |
| 10. | Maduka ya dawa muhimu ya binadamu au mifugo. | 5,000/= |
| 11. | Zahanati au Kliniki na Vituo vya Afya vya Taasisi na watu binafsi. | 10,000/= |
| 12. | Maeneo ya biashara yaliyofungwa baada ya ukaguzi wa awali na kuomba kufanyiwa ukaguzi mpya | 7,000/= |
| 13. | Duka au kibanda cha biashara ya jumla. | 3,000/= |
| 14. | Ukaguzi wa Vioski. | 2,000/= |
| 15. | Majengo ya taasisi binafsi. | 10,000/= |
| 16. | Vyoo vya kibiashara vinavyoendeshwa na watu binafsi. | 3,000/= |
| 17. | Karakana na gereji za magari na mitambo. | 3,000/= |
| 18. | Karakana za vyuma na viwanda vya mbao. | 2,000/= |
| 19. | Mtoa tiba Asilia. | 2,000/= |
| 20. | Saluni ya kiume na kike. | 2,000/= |
| 21 | Ada ya kibali cha tiba mbadala au asilia | 50,000/= kwa kila mwaka. |

## SEHEMU YA XII: ADA YA HUDUMA ZA ARDHI

(A) Ada na Vibali vya Ujenzi

| Namba. | Aina ya Jengo | Gharama (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Jengo la makazi na biashara ya maduka | 25,000/= kwa kibali. |
| 2 | Jengo la makazi ghorofa moja | 50,000/= kwa kibali. |
| 3 | Jengo la makazi na biashara | 150,000/= kwa kibali. |
| 4 | Jengo la biashara | 200,000/= kwa kibali. |
| 5 | Jengo la biashara zaidi ya ghorofa moja | 250,000/= kwa kibali. |
| 6 | Jengo la kiwanda | 85,000/= kwa kibali. |
| 7 | Jengo la taasisi binafsi | 500,000/= kwa kibali. |
| 8 | Ujenzi wa mnara | 2,000,000/= kwa kibali. |
| 9 | Ada ya maombi ya upimaji wa Ardhi | 20,000/= kwa kila kiwanja. |
| 10. | Ada ya kubadili matumizi ya kiwanja | 20,000/= kwa kibali |

(B) Ada Nyinginezo

| Namba. | Kazi | Aina | Ada (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuweka Uzio wa kiwanja. | Bati au ukuta. | 100/=kwa futi (Kulingana na | Wiki Mbili hadi Mwaka |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | muda na eneo ambapo uzio utawekwa,) | mmoja. |

(C) Ada ya Vibali vya Ukarabati wa Majengo

| Namba. | Kazi | Aina | Ada (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ukarabati | Nyumba za watu binafsi | 10,000/= kwa kila kibali. |
| | | Taasisi binafsi | 20,000/= kwa kila kibali. |
| 2 | Ukarabati au kibali kilichopita muda ulioombewa | Nyumba za watu binafsi | 30,000/= kwa kila kibali. |
| | | Taasisi binafsi | 50,000/= kwa kila kibali. |

(D) Ada ya maombi ya kupatiwa maelekezo ya kiupangaji

| Namba | Eneo la makazi lisilo na msongamano | Eneo la makazi lenye msongamano wa kati | Eneno la makazi lenye msongamano |
|---|---|---|---|
| 1 | 30,000/= | 25,000/= | 20,000/= |
| 2 | Huduma zingine | | |
| | Viwanda | Ukubwa wa Eneo | Ada ya Maombi (Shilingi) |
| | (i)Viwanda vya Huduma | Mita za Mraba 1,500 hadi 4,000 | 40,000/= |
| | (ii)Viwanda vya kati | Mita za Mraba 4,001 hadi 8,000 | 80,000/= |
| | (iii)Viwanda Vikubwa | Mita za Mraba zaidi ya 8,000 | 200,000/= |
| 3. | Mashamba | Ukubwa wa Eneo (Ekari) | Ada ya Maombi (Shilingi) |
| | i)Mashamba madogo | 1 hadi 2 | 20,000/= |
| | (ii)Mashamba ya kati | 2.5 hadi 4 | 50,000/= |
| | (iii)Mashamba makubwa | 4.5 hadi 10 | 100,000/= |
| | (iv)Mashamba makubwa zaidi | zaidi ya 10 | 250,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 918 (Linaendelea)*

| 4 | Taasisi binafsi | Ukubwa wa eneo | Ada ya Maombi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| | (i)Shule ya awali | | 30,000/= |
| | (ii) Shule ya msingi | | 50,000/= |
| | (iii) Shule ya sekondari na vyuo | | 80,000/= |
| 5 | Afya | Ukubwa wa eneo | Ada ya Maombi (Shilingi) |
| | (i)Zahanati | | 25,000/= |
| | (ii)Kituo cha Afya | | 50,000/= |
| | (iii)Shule ya Awali | | 100,000/= |
| 6 | Maeneo ya Kuabudia na Kumbi mbalimbali | Ukubwa wa eneo | Ada ya Maombi (Shilingi) |
| | (i)Msikiti | | 30,000/= |
| | (ii)Kanisa | | 30,000/= |
| | (iii)Kituo cha maombi | | 50,000/= |
| | (iv)Kumbi mbalimbali | | 30,000/= |
| 7 | Ofisi Mbalimbali | Ukubwa wa eneo | Ada ya Maombi (Shilingi) |
| | (i) Taasisi binafsi | | 50,000/= |
| | (ii)Vituo vya mafuta | | 150,000/= |
| | (iii)Makazi maalum | | 50,000/= |
| | (iv)Hoteli | | 50,000/= |
| | (v)Hosteli | | 50,000/= |
| | (vi)Nyumba za kulala wageni | | 50,000/= |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (vii)Upimaji na Uuzaji wa viwanja | | 200,000/= |
| | (viii)Makazi ya familia zaidi ya moja | | 50,000/= |

SEHEMU YA XIII: ADA ZA MAOMBI YA ZABUNI MBALIMBALI ZA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya chanzo | Kiasi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ukusanyaji wa mapato | 50,000/= |
| 2. | Ujenzi wa barabara | 100,000/= |
| 3. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu (CBD) | 50,000/= |
| 4. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu (pembezoni) | 50,000/= |
| 5. | Kupakua mashimo ya maji taka (vyoo) | 50,000/= |
| 6. | Kukarabati na kujenga maduka Vioski na vizimba vya umma | 50,000/= |
| 7. | Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo) | 50,000/= |
| 8. | Ukaguzi na upimaji wa viwanja. | 100,000/= |
| 9. | Uendeshaji vyoo vya umma | 50,000/= |
| 10. | Uendeshaji wa vioski vya Halmashauri | 20,000/= |
| 11. | Huduma elekezi / mshauri (Consultancy services) | 50,000/= |
| 12. | Upangishaji Maduka / Vizimba | 20,000/= |
| 13. | Ujenzi wa majengo | 50,000/= |
| 14. | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalamu (non-consultancy services) | 50,000/= |
| 15. | Maeneo mengine ambayo hayajatajwa | 20,000/= |

SEHEMU YA XIV: USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Tofali | |
| | (i) Gari ya ujazo wa tani 1 hadi 5 | 3,000/= kwa tripu. |
| | (ii) Gari ya ujazo wa tani 6 hadi 10 | 5,000/= kwa tripu. |
| | (iii) Gari ya ujazo wa tani 10 hadi 15 | 7,000/= kwa tripu. |
| | (iv) Gari ya ujazo wa tani 16 na kuendelea | 10,000/= kwa tripu. |
| 2. | Udongo | |
| | (i) Gari ya ujazo wa tani 1 hadi 5 | Tshs 1,000/= kwa tripu. |

*Tangazo La Serikali Na. 918 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | (ii) Gari ya ujazo wa tani 6 hadi 10 | Tshs 2,000/= kwa tripu. |
| | (iii) Gari ya ujazo wa tani 10hadi 15 | Tshs 3,000/= kwa tripu. |
| | (iv) Gari ya ujazo wa tani 16 na kuendelea | Tshs 4,000/= kwa tripu. |
| 3 | Mawe au Moramu au Mchanga au Kokoto ya ujazo | |
| | (i) Gari ya ujazo wa tani 1 hadi 5 | 2,5000/= kwa tripu. |
| | (ii) Gari ya ujazo wa tani 6 hadi 10 | 3,500/= kwa tripu. |
| | (iii) Gari ya ujazo wa tani 10 hadi 15 | 5,000/= kwa tripu. |
| | (iv) Gari ya ujazo wa tani 16 na kuendelea | 6,000/= kwa tripu. |
| 4 | Chokaa na aina nyingenezo za namna hiyo | 300/= kwa mfuko wa kilo 25. |
| 5 | Ada ya ukaguzi wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi | 100,000/= kwa kila maombi yatakayo kaguliwa. |
| 6 | Ada ya umiliki wa eneo linalochimbwa madini ya ujenzi | 500,000/= kwa kila mwaka. |

SEHEMU YA XV: USHURU WA SOKO GULIO NA MINADA

| Namba. | Aina ya chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kwenye masoko | 500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 2. | Vizimba | 500/= kwa siku au kitambulisho cha Mjasiliamali. |
| 3. | Kuuza nguo za mitumba kwenye gulio au minada | 1,500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 4. | Kuuza nguo mpya kwenye gulio au mnada | 1,000/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 5. | Mama na Baba lishe | 500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 6. | Kuuza nyama ya ng’ombe kwenye gulio au mnada, mbuzi na kondoo | 5,000/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 7. | Kuuza nyama ya mbuzi, kondoo na kuku au jamii nyingine ya ndege kwenye gulio au mnada, | 3,500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 8. | Kuuza Vyombo vya ndani kwenye gulio au mnada | 1,000/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Banda la kuuzia kuku sokoni, gulioni au mnadani | 500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 10. | Uuzaji wa pumba | 500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 11. | Bidhaa za urembo | 500/= kwa siku au kitambulisho cha mjasiliamali. |
| 12. | Bidhaa zinginezo | 500/= mpaka 1,000/= kwa siku. |
| 13. | Kibali cha kusafirisha mazao | 2,000/= kwa kila kibali. |
| 14. | Ushuru wa kuuza gulioni na minada | 500/= kwa siku. |

SEHEMU YA XVI: USHURU WA MAJI

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Gari kubwa au Boza linalobeba ujazo wa lita 501 hadi 20,000 | 10,000/= kwa tripu. |
| 2 | Kenta au gari dogo la mizigo linalobeba ujazo wa lita 3001 hadi 5000 | 3,000/= kwa tripu. |
| 3 | Mkokoteni unaobeba ujazo wa lita 100 hadi 3000 | 1,000/= kwa tripu. |

SEHEMU YA XVII: USHURU WA HUDUMA

| Namba. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Kwa Taasisi za shule na huduma za Afya kwa sekta binafsi | 500,000/= kwa mwaka. |
| 2. | Makampuni ya aina zote | 200,000/= kwa mwaka. |
| 3. | Biashara nyinginezo zisizo na VAT | 100,000/= kwa mwaka. |

SEHEMU YA XVIII: ADA YA HUDUMA YA UKUSANYAJI NA UZOAJI WA TAKA

| Namba. | Aina ya Biashara au mchangiaji | Kiwango cha Ada kwa Mwezi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Mgahawa mdogo au kibanda cha kuuzia chai au chakula. | 3,000/= |
| 2. | Kioski na Glosari. | 3,000/= |
| 3. | Nyumba ya kulala wageni | 5, 000/= |
| 4. | Zahanati (Taka zisizo hatari). | 10, 000/= |
| 5. | Kituo cha Afya (Taka zisizo hatari). | 15, 000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 918 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Fundi Seremala. | 3,000/= |
| 8. | Fundi chuma. | 2, 000/= |
| 9. | Karakana au gereji za magari. | 5,000/= |
| 10. | Karakana nyinginezo. | 5,000/= |
| 11. | Duka la jumla | 5,000/= |
| 12. | Duka la reja-reja. | 3,000/= |
| 13. | Duka dogo la vyakula. | 2, 000/= |
| 14. | Duka kubwa la vyakula. | 3,000/= |
| 15. | Baa | 3,000/= |
| 16. | Kumbi za Starehe au disko | 10,000/= |
| 17. | Duka la kuuza samaki au nyama (bucha ya samaki au nyama) | 3,000/= |
| 18. | Kibanda au kituo cha nyama choma au chipsi kinachojitegemea | 2,000/= |
| 19. | Duka la Dawa (Jumla na reja—reja) | 2,000/= |
| 20. | Duka la dawa la reja—reja | 2,000/= |
| 21. | Kiwanda kidogo au kiwanda cha kati | 10, 000/= |
| 22. | Fundi cherehani | 2,000/= |
| 23. | Saluni ya wanaume au wanawake | 3,000/= |
| 24. | Kibanda au mwamvuli wa kuuza vocha za simu eneo la Hifadhi la Ardhi la Halmashauri ya Wilaya. | 2,000/= |
| 25. | Kituo cha Kuuzia nishati ya mafuta | 10,000/= |
| 26. | Washona viatu | 2,000/= |
| 27. | Wauza viatu vya mitumba/ dukani | 2,000/= |
| 28. | Wauza nguo za mitumba | 2,000/= |
| 29. | Toroli la bidhaa au matunda | 2,000/= |
| 30. | Stoo za mkaa | 5,000/= |
| 31. | Stoo za mbao | 5,000/= |
| 32. | Mama au Baba lishe | 2,000/= |
| 33. | Duka la kuuzia vipuli vya magari | 3,000/= |
| 34. | Kila kaya | 500/= |
| 35. | Kila meza au kizimba ndani ya soko | 2,000/= |
| 36. | Ofisi za Taasisi kama benki au posta na tasisi nyingine za kifedha. | 10,000/= |
| 37. | Steshenari au maduka ya kuuza vitabu | 5,000/= |
| 38. | Duka la dawa muhimu za binadam au duka la dawa za mifugo au pembejeo za kilimo | 3,000/= |
| 39. | Hospitali au vituo vya Afya au zahanati za watu binafsi | 10,000/= |
| 40. | Vyuma chakavu tani moja | 12,000/= |

SEHEMU YA XIX: GHARAMA ZA UTUPAJI TAKA KWENYE JALALA (JAA) LA TAKA LA HALMASHAURI

| Namba. | Kiasi cha Taka | Ada kwa Mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Taka za aina yoyote kwa kiwango cha ujazo | 30,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | chini ya tani moja. | |
| 2 | Taka za aina yoyote kwa kiwango cha ujazo tani moja. | 50,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi…………...…. Mwaka ………...… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya ……………ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: …………………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Kibondo imebandikwa kwenye sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo uliofanyika Tarehe 31 mwezi 01 Mwaka 2023

DIOCLES M. RUTEMA
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo*

HABILI C. MASEKE
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*